

## **WATOTO wasioona Songea wanakabiliwa na changamoto lukuki Na Albano Midelo**

KITENGO cha watoto walemvu wasioona Luhira katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea Mkoa wa Ruvuma, ndiyo kitengo pekee kwa ajili ya wasioona ukanda wa kusini kikiwa kinakabiliwa na changamoto mbalimbali.



Kitengo hicho ambacho ni ukombozi kwa watoto wasioona nchini kilianzishwa mwaka 1982,hata hivyo shule ya msingi Luhira ni mionganoni mwa shule kongwe nchini ilianzishwa mwaka 1929.

Mkuu wa kitengo hicho ambaye pia ni mlemavu wa macho mwalimu Salum Hapendeki anasema kitengo hicho Kina wanafunzi wenye ulemavu wasioona 42 kati yao wavulana 20 na wasichana 22 kati yao watoto wenye ulemavu wa ngozi ni saba na kwamba uwezo wa kitengo hicho ni kuchukua wanafunzi wasioona 60.

“Tunashindwa kuchukua wanafunzi 60 wasioona kutokana na shule yetu ambayo ni ya bweni inakabiliwa na upungufu mkubwa wa vitanda na magodoro,katika mkoa wa Ruvuma pekee kuna

watoto wengi wasioona wenyе umri wa kwenda shule ambao hawasomi”, anasema.

Hata hivyo Hapendeki anaishukuru Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa TAMISEMI ambayo inatoa fedha kila mwaka katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea kwa ajili ya kuendeshea elimu maalum na kwamba Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma ametoa magodoro kupunguza changamoto ya uchakavu wa magodoro katika shule hiyo.

Anasema kitengo hicho kinanufaika ambapo kila mwezi kinapata ruzuku ambayo inatumika kwa ajili ya chakula, usafiri na vifaa vya kujifunzia na kufundishia.

“TAMISEMI kupitia Halmashauri ya manispaa ya Songea pamoja na wadau wengine wa elimu kama vile Mamlaka ya Elimu Tanzania TEA inatoa fedha na vifaa kwa mfano katika shule yetu tumepewa fimbo nyeupe za kuongezea wasioona na mashine maalum ya photocopy aina ya thermoform kwa ajili ya wasioona yenyе thamani ya sh. milioni 18 inatusaidia sana”, anasisitiza.

Hata hivyo Hapendeki anataja changamoto zinazoikabili shule hiyo kuwa ni karatasi maalum yaani rim ambazo zinatumika kwa ajili ya wasioona zinapatikana jijini Dar es salaam pekee kwa sh.laki tatu bei ambayo ni kubwa ukilinganisha na rim za karatasi za kawaida.

Changamoto nyingine ni ukosefu wa umeme wa uhakika hali ambayo inahatarisha ulinzi na usalama wa watoto hao na walimu kushindwa kutumia vifaa vya kufundishia na kujifunzia vinavyotumia umeme hivyo kuchangia kushusha elimu kwa watoto wenyе ulemavu.

Langson Mtega Mwalimu asiyeona anasisitiza kuwa katika Mkoa wa Ruvuma kuna watoto wasioona ambao hawasomi ambao wamekosa msaada wa kufikishwa katika shule hiyo ili kupata elimu ambayo ni ukombozi katika maisha yao.

Licha ya changamoto zinazokikabili kitengo hicho, kitaaluma kila mwaka wanafunzi wasioona katika kitengo hicho wanamudu kufanya vizuri mtihani wa Taifa wa darasa la saba kwa mfano mwaka juzi kati ya wanafunzi watano waliofanya mtihani wanafunzi wanne walifaulu na kuendelea na masomo ya sekondari na mwaka jana wanafunzi wote wawili walichaguliwa kuendelea na elimu ya sekondari.

Afisa Elimu Maalum katika Manispaa ya Songea Rehema Nyagawa anasema shule hiyo pia inakabiliwa na upungufu wa matundu ya vyoo hali ambayo inasababisha watoto wa kiume kujisaidia choo kimoja na walimu, shule ina majengo chakavu ambayo ni mabweni, jiko na bwalo la chakula na uchakavu wa magodoro na vitanda.

Changamoto nyingine anaitaja kuwa ni, watoto wenye ulemavu wa ngozi hawana mafuta maalum ya ngozi na shule haina usafiri wa uhakika kwa ajili ya wanafunzi wanapouguwa usiku au ziara za kimasomo.



Mkuu wa Wilaya ya Songea Pololet Mgema ameahidi kutafutia

ufumbuzi matatizo yanayoikabili shule hiyo ya watoto wasioona.

Ulemavu wa macho unatokana na magonjwa ya macho ambayo hapa nchini yanatishia ustawi wa jamii kutokana na takwimu kuonesha kuwa idadi ya wagonjwa wenyewe matatizo ya kutoona na uoni hafifu kuongezeka kwa kasi kubwa.

Baadhi ya sababu zinazosababisha upofu ni mtoto wa jicho unaosababisha upofu kwa asilimia 50,kovu kwenye kioo cha jicho,upungufu wa vitamin A na surua ambayo inasababisha upofu kwa asilimia 20.

Kwa mujibu wa takwimu za shirika la Afya Duniani (WHO) Tanzania inakadiriwa kuwa na watu 450,000 wasioona na wengine takriban 1,350,000 wana uoni hafifu.

Kulingana na WHO Inakadiriwa kuwa takribani watu milioni 285 duniani wana matatizo ya kuona,kati ya hao wenyewe upofu ni milioni 39 na 246 wana uoni hafifu.China pekee ina idadi ya watu wasioona milioni 12.

**Albano Midelo ni Mchangiaji wa gazeti hili unaweza kuwasiliana kwa baruapepe: [albano.midelo@gmail.com](mailto:albano.midelo@gmail.com),simu 0784765917**